

Burundi kukutana na waasi waliojitoa

5 May 2004

The Guardian

BUJUMBURA, Burundi

SERIKALI ya Burundi imesema itakutana na waasi waliojiondoa serikalini na katika bunge ili kuangalia sababu za kujiondoa kwao na namna wanavyoweza kurejea.

Chama cha waasi cha FDD kilitangaza Jumatatu kujiondoa katika serikali ikipinga namna serikali inavyofanya vitu vyake.

Serikali hiyo ya Burundi imesema kwamba itaangalia madai ya waasi hao ya magavana na watawala wa wilaya na itatumia nafasi hiyo kuwashawishi kurejea katika serikali.

Wakati wakijitoa walisema kwamba serikali ya Kitusti na Wapinzani wao wa Kihutu walikuwa hawatekelezi makubaliano yaliyomaliza vita vya muongo mmoja.

Wachambuzi wa mambo wamesema kwamba nchi hiyo imesimama tena na kuingia katika hatari ya kuelekea katika kiza cha mauti baada ya waasi hao kujiondoa serikalini.

Taifa hilo la Burundi lenye watu milioni 6.5 limekuwa vitani kwa miaka 10 na kusababisha vifo na uharibufu mkubwa wa mali.

"Tumeamua kusimamisha ushiriki wetu katika serikali na katika bunge mpaka hapo usitishaji wa mapigano utakapokuwa timilifu," alisema Hussein Rajabu, Katibu mkuu wa chama cha Forces for the Defence of Democracy (FDD), wakati akizungumza na Reuters juzi Jumatatu.

Amesema hata hivyo kwamba maamuzi hayo hayana maana kwamba wanarejea katika vita, lakini kama wafuasi wake wafashambuliwa watajibu mapigo.

Waasi hao wa Kihutu wamekuwa wakipigana na jeshi la Burundi lenye Watutsi wengi toka mwaka 1993 katika jaribio la kuondoa mamlaka ya Watutsi ambao ni wachache.

Vita hiyo imeua watu 300,000. Mtaalamu wa masuala ya Burundi Bw. Jan Van Eck, kutoka taasisi ya masuala ya usalama ya Pretoria- Institute for Security Studies- amesema huo ni mwenendo mbaya na unaonyesha kugawanyika kwa serikali.

Chama hicho cha FDD kilijiunga na serikali ya mseto Novemba mwaka jana kwa matumaini ya kuleta amani nchini Burundi.

Katika makubaliano chama hicho kina mawaziri wanne na wabunge 15 katika bunge lenye wabunge 190.

Lakini Rajabu amesema kwamba FDD inasubiri kupatiwa asilimia 30 za magavana wa majimbo na tawala za wilaya - nafasi zenye mamlaka makubwa katika serikali- ambazo waliahidiwa wakati wa kutia saini mkataba wa kusitisha mapigano.

Askari kutoka jeshi la kulinda amani la Afrika nchini Burundi wanawalinda viiongozi wakuu wa FDD wakati askari wao wanaingizwa katikajeshi la Burundi.

Rajabu amesema kwamba maamuzi ya kujiondoa serikalini haitaathiri programu ya kutumbukiza wapiganaji wake wa FDD katika jeshi jipya.

"Hatuna matatizo na watu waliozoea kupigana. Tuna matatizo na wanasiasa na vyama vyao vya saasa," alisema Bw. Rajab.

Mchambuzi Van Eck amesema kwamba Burundi, taifa lenye historia ya mauaji ya kutisha kwa miaka 40 iliyopita, inahitaji msaada mkubwakuzuia ufa unaotaka kutanuka kuhusiana na amani iliyopatikana.

"Hali inaonyesha kuwa suala la Burundi bado kuisha," alisema.

Serikali ya mpito bado inapigana vita na na kundi jingine la Kihutu lenye msimamo mkali la Forces for National Liberation.

Vurugu zinazoendelea sasa zinatishia uchaguzi mkuu kwa mujibu wa makubaliano ya mwaka 2000.